# CHRISTIANS IN

# *The*

# BUSINESS WORLD 2

**PASTOR TONY OSBORN**

**© July 2024 Pastor Tony Osborn**

Kitabu hiki kimeandikwa na **PASTOR TONY OSBORN**. Haki zote zimehifadhiwa, huruhusiwi kunakili, kurudufu au kutumia sehemu ya kitabu hiki bila idhini ya mwandishi.

Kufanya hivyo itakuwa ni ukiukwaji wa taratibu na hii inaweza kukupelekea kushtakiwa kutoka kwa waandaaji wa kazi hii.

**Pastor, Tony Osborn**

**Dar es salaam, TANZANIA (Afrika Mashariki)**

**Simu: 0762153539/0659085731**

**Instagram / Tiktok: Pastor Tony Osborn**

**ISBN: 978-9912-9873-3-3**

# YALIYOMO:

**SHUKRANI:** .......... vii

**UTANGULIZI:** .......... ix

**Sura ya 1:**

**UFAHAMU WA BIASHARA** .......... 13

1.1 BIASHARA NI NINI? .......... 14

1.2 MKRISTO NA BIASHARA .......... 15

1.3 TOFAUTI KATI YA MFANYABIASHARA MKRISTO NA WA KAWAIDA .......... 18

1.4 KWANINI WAKRISTO WENGI HAWAONI MAFANIKIO KATIKA BIASHARA ZAO? .......... 21

1.5 NAFASI YA MUNGU KATIKA BIASHARA YAKO .......... 37

a) Mungu kama mshirika wa kwanza wa biashara yako. .......... 38

b) Mungu kama kiongozi .......... 39

c) Mungu kama mmiliki halali wa biashara yako. .......... 42

d) Mungu kama mwalimu na mshauri mkuu. .......... 43

1.6 FAIDA YA UWEPO WA MUNGU KATIKA BIASHARA YAKO .......... 43

1.7 MAMBO YA MSINGI YA KUZINGATIA KABLA HUJAANZA BIASHARA .......... 47

**Sura ya 2:**

**KANUNI ZA KIROHO ZA KUFANIKIWA KIBIASHARA** .......... 53

2.1 Kanuni ya 1: Sadaka .......... 54

2.2 Kanuni ya 2: Kufunga na kuomba kwa ajili ya biashara yako .......... 66

2.3 Kanuni ya 3: Roho ya Ufunuo .......... 68

2.4 Kanuni ya 4: Roho ya hekima, maarifa na ujuzi. .......... 71

2.5 Kanuni ya 5: Roho ya Ubora .......... 74

2.6 Kanuni ya 6: Imani iliyoambatana na matendo .......... 78

2.7 Kanuni ya 7: Roho ya kibali juu yako. .......... 81

- Kibali cha Kuonekana (Kibali cha Esta) .......... 82
- Kibali cha Kukubalika (Kibali cha Danieli) .......... 84
- Kibali cha kuvuta wateja (Kibali cha Daudi) .......... 86
- Kibali cha kuuza .......... 87
- Kibali cha ushawishi. .......... 89

2.8 Kanuni ya 8: Uongozi wa Roho Mtakatifu .......... 92

2.9 Kanuni ya 9: Neno la Mungu .......... 94

2.10 Kanuni ya 10: Nuru /Utukufu wa Mungu kuwa juu yako .......... 96

2.11 Kanuni ya 11: Utakatifu .......... 103

**Sura ya 3:**

**SIRI ZA KUKUA KIBIASHARA .......... 111**

3.1 Kuwa na uwezo wa kutatua matatizo ya watu. .......... 112

3.2 Kuwa na watu sahihi katika biashara yako .......... 119

3.3 Roho ya uendelevu bila kukata tamaa .......... 120

3.4 Upako wa kukua kwa kasi kwenye biashara yako (Anointing of speed) .......... 124

**Sura ya 4:**

**MAHUSIANO NA BIASHARA .......... 125**

4.1 NAFASI YA MPENZI KATIKA MAENDELEO YA BIASHARA .......... 126

4.2 MAHUSIANO YA NDUGU NA RAFIKI KATIKA BIASHARA YAKO .......... 129

4.3 HATARI YA KUCHANGANYA MAHUSIANO NA BIASHARA ........................................................................................ 133

4.4 MAMBO YA MSINGI YA KUZINGATIA KABLA HUJAAJIRI RAFIKI, NDUGU AU MPENZI ...................................................... 138

**Sura ya 5:**

**MUONGOZO WA MAOMBI WA KUOMBEA BIASHARA ZETU 142**

5.1 Maombi ya kibali juu ya Biashara zetu ............................................ 143

5.2 Maombi ya Biashara zetu kuonekana na watu .................................. 144

5.3 Maombi ya kuvuta na kuwaleta wateja katika biashara yako ............. 145

5.4 Maombi ya ulinzi juu ya Biashara zetu ............................................ 146

5.5 Maombi ya kuombea kila mteja anayekuja dukani kwako ili arudi tena ........................................................................................ 148

5.6 Maombi ya Neema ya kukua na kuongezeka katika biashara ........... 150

5.7 Kuomba Baraka ya Bwana kuwa juu ya Biashara yako ..................... 151

5.8 Kuomba Roho ya ubora kuwa juu yako .......................................... 154

5.9 Kuomba neema ya kuuza na kupata faida ........................................ 155

5.10 **Kuomba hekima, maarifa na ujuzi wa kipekee katika kufanya biashara yako ..................................................................** 156

5.11 kuomba usaidizi wa Roho Mtakatifu katika biashara yako ............. 158

5.12 Maombi ya shukrani................................................................... 159

**Sura ya 6:**

**MATENDO YA KIIMANI KWA AJILI YA WAFANYABIASHARA ........................................................................................ 160**

6.1 TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA KARATASI .................. 161

6.2 TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA UDONGO ..................... 165

6.3 TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA MSHUMAA .................. 167

6.4 TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA CHUMVI NA MAJI ...... 173
**HITIMISHO ........................................................................................ 175**
**SALA YA WOKOVU/ KUMPOKEA YESU ....................................... 176**
**MAELEKEZO NAMNA YA KUTUMA SADAKA YAKO NA KUJIUNGA NA PARTNERSHIP ........................................................ 178**

# SHUKRANI:

Ninamshukuru Mungu sana kwa uaminifu wake na kwa kunijalia ROHO MTAKATIFU ambaye kwa mafunuo yasiyo ya kawaida amenipa NEEMA ya kuandika kitabu hiki kilichobeba mafunuo na siri nyingi sana juu ya somo zima la biashara na kutoa mbinu na kanuni za kiroho ambazo zitawasaidia wakristo wote walio katika biashara kufanikiwa na kuongezeka.

Siri na maombi niliyoyaandika humu kwa uwezo wa Roho wa Mungu zitakusaidia na kukuongoza hatua kwa hatua kukuvusha na kukusaidia kukua katika biashara yako na kupata mafanikio ambayo umekuwa ukitamani kuyapata.

Neno la Mungu linasema katika kitabu cha;

***Kumbukumbu la torati 8:18***

***"Bali utamkumbuka BWANA, Mungu wako, maana ndiye akupaye nguvu za kupata utajiri; ili alifanye imara agano lake alilowapa baba zako, kama hivi leo."***

Kwahiyo kupitia kitabu hiki Mungu atakusaidia na kukupa nguvu, hekima na maarifa ambayo yatakusaidia kupata mafanikio kifedha hadi kufikia utajiri kupitia biashara yako.

Shukrani zangu za pekee ziwafikie watoto wangu wa kiroho wote, ndani na nje ya nchi ya Tanzania, kwa kunipenda, kuniombea na zaidi ya yote kunipokea na kuniamini na kumuamini Mungu aliyeniita na huduma iliyopo ndani yangu. Ninawashukuru sana kwa kuwa nyie mmenipa nafasi katika mioyo yenu na kuamini huduma ambayo Mungu ameiweka ndani yangu.

Ninawapenda, ninawaombea na Mungu wa mbinguni awabariki sana.

Kiupekee kabisa ninamshukuru mke wangu mpenzi Mrs Neema Tony Kapola ambaye amekuwa akikesha pamoja nami, akisukuma na kusimamia kwa ufasaha ukamilifu wa kitabu hiki. Ninakupenda na Asante kwa kusimama na mimi katika wito na kazi hii ambayo Mungu amenipa.

Mungu aendelee kukuonekania wewe na familia yako ndani ya mwaka huu.

*Amen……………………*

***~Pastor Tony Osborn***

# UTANGULIZI:

Kitabu hiki cha **“CHRISTIANS IN THE BUSINESS WORLD”** ni kitabu kilichojaa hekima na maarifa na mafundisho ya kimungu juu ya eneo zima la biashara na mafanikio kuchumi kupitia biashara.

Jambo nililogundua ni kuwa; watu wengi sana katika karne hii wamejikita katika kujiajiri kupitia biashara na ujasiriamali na kati ya watu hao wakristo ni moja ya watu ambao pia hujihusisha katika biashara. Lengo kubwa la kuandika kitabu hiki ni kuwasaidia wakristo wote na kuwapa muongozo sahihi wa namna ya kupata mafanikio katika biashara zao.

Watu wa huku duniani wao wana njia zao na mbinu zao ambazo huwa zinawasaidia katika kufanikiwa kibiashara. Wapo wanaoua mama zao na watoto wao ili wafanikiwe kibiashara, wapo wanaotoa sadaka kwa miungu mingine ili wafanikishwe kibiashara na wapo ambao wanaenda kwa waganga ili tu wapate mafanikio ya kibiashara. Sasa watu wa duniani wana njia zao na sisi watu wa Rohoni au wakristo tuna njia zetu ambazo kama tukizitumia hizo tutaona na kupata mafanikio makubwa sana katika biashara zetu.

Kabla hatujaenda mbali zaidi kuna maswali baadhi ambayo nilijiuliza kwa undani kabla sijaandika kitabu hiki.

~Ni kwanini wakristo wafanye biashara?

~Kwanini sisi tuwe matajiri?

~Ni kwanini sisi wakristo inatupasa kuwa na nguvu ya kiuchumi?

Ukisoma katika Biblia watumishi wengi wa Mungu walikuwa na nguvu kiuchumi. Wengi Mungu aliwapa kumiliki ng'ombe, mifugo, fedha na mali nyingi sana. Baadhi ya watumishi hawa wa Mungu ni pamoja na Ibrahimu, Yakobo, Suleiman, Yusufu, Ayubu na wengineo.

Kwahiyo kuokoka au kuwa upande wa Mungu sio sababu ya sisi kuishi maisha duni kama wengi wanavyoamini katika jamii zetu kuwa; walokole wengi huwa maskini. Wengi ni maskini na hawana mafanikio kwa sababu hawafuati sheria na kanuni zao kama watu wa dunia hii wanavyofata sheria na kanuni za ufalme wao. Kuwa tajiri na nguvu ya kumiliki ni mpango wa Mungu mwenyewe tangu anamuumba mwanadamu. Tunaona katika kitabu cha;

**Mwanzo 1:26-28**

**"Mungu akasema, na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba."**

Kwahiyo sisi tulipewa nguvu ya kumiliki na kutawala vyote vilivyopo nchi kavu na baharini na hivyo ni haki yetu kufanikiwa kibiashara maana nguvu hiyo ya kumiliki na kutawala imo ndani yetu. Lakini ili tuweze kuyaona hayo mafanikio ni lazima tufuate sheria na kanuni zote za kiroho za kutusaidia kufanikiwa ambazo kitabu hiki kimeziandika siri hizo na kanuni hizo kwa undani kabisa.

Tunasoma katika kitabu cha;

**Hagai 2:4-8**

**“Lakini sasa uwe hodari, Ee Zerubabeli, asema BWANA; nawe uwe hodari, Ee Yoshua, mwana wa Yehosadaki, kuhani mkuu, nanyi iweni hodari, enyi watu wote wa nchi hii, asema BWANA; mkafanye kazi, kwa kuwa mimi ni pamoja nanyi, asema BWANA wa majeshi; kama neno lile nililoagana nanyi mlipotoka katika nchi ya Misri; na roho yangu inakaa kati yenu; msiogope.**

**Kwa maana BWANA wa majeshi asema hivi, Mara moja tena, ni kitambo kidogo tu, nami nitazitikisa hizo mbingu, na hii nchi, na bahari, na nchi kavu; nami nitatikisa mataifa yote, na vitu vinavyotamaniwa na mataifa yote vitakuja; nami nitaijaza nyumba hii utukufu, asema BWANA wa majeshi. Fedha ni mali yangu, na dhahabu ni mali yangu, asema BWANA wa majeshi.”**

Tukisoma katika kitabu hiki tutagundua kuwa, Mungu mwenyewe ndiye aliyetoa maagizo kuwa watoto wake wakafanye kazi, wakafungue biashara, wakafungue makampuni na wakajiajiri kwa sababu Mungu atakuwa na wao na atawafanikisha maana fedha na dhahabu ni mali ya Mungu.

Hivyo sababu nyingine inayotufanya sisi wakristo tukafanye kazi na tuingie katika biashara ni kwa sababu ni agizo la Mungu mwenyewe na tuna uhakika wa ahadi ya Mungu kuwa atakuwa pamoja na sisi.

Ukiachana na kuwa ni agizo la Mungu sisi kama wakristo tunaishi duniani na duniani kuna mifumo mingi ambayo inayotuwezesha sisi kuishi vizuri ambayo mifumo hii inahitaji sisi kuwa na fedha. Ijapokuwa duniani sisi tunapita bado tunahitaji kuwa na nguvu ya

kiuchumi ili tuweze kuishi vizuri kabla ya unyakuo wa kwenda mbinguni.

Ndani ya kitabu hiki utajifunza juu ya;

- ❖ Kanuni za kiroho ambazo wewe kama mfanyabiashara mkristo zitakusaidia kufanikiwa na kuona matokeo makubwa.
- ❖ Siri za kiroho zitakazokuwezesha kufanikiwa katika eneo la biashara.

Pamoja na kujifunza mambo haya ya msingi nimeambatanisha kitabu hiki na muongozo wa maombi ambayo wewe binafsi utayatumia kwa ajili ya kuombea biashara yako kwa undani.

Jambo ambalo huwa nawafundisha sana wanangu wote wa kiroho ni kuwa na uwezo wa kujiombea wenyewe bila kumsubiria mchungaji au nabii. Kwahiyo maombi yaliyomo katika kitabu hiki ni maombi ambayo yatakusaidia sana katika kutafuta na kupata matokeo mazuri katika biashara yako kila siku.

Zaidi ya yote Mungu akubariki sana na akakufanikishe sana katika kazi ya mikono yako na biashara yako kama Neno la Mungu linavyosema katika kitabu cha;

**Kumbukumbu la torati 28:3-6**

**"Utabarikiwa mjini, utabarikiwa na mashambani. Utabarikiwa uzao wa tumbo lako, na uzao wa nchi yako, na uzao wa wanyama wako wa mifugo, maongeo ya ng'ombe wako, na wadogo wa kondoo zako. Litabarikiwa kapu lako, na chombo chako cha kukandia unga. Utabarikiwa uingiapo, utabarikiwa na utokapo."**

# 1

*Sura ya Kwanza*

# UFAHAMU WA BIASHARA

**"Lakini sasa uwe hodari, Ee Zerubabeli, asema BWANA; nawe uwe hodari, Ee Yoshua, mwana wa Yehosadaki, kuhani mkuu, nanyi iweni hodari, enyi watu wote wa nchi hii, asema BWANA; mkafanye kazi, kwa kuwa mimi ni pamoja nanyi, asema BWANA wa majeshi;"**

**Hagai 2:4**

## 1.1 BIASHARA NI NINI?

Ukisikia neno biashara nini hasa kinakuja kwenye akili yako? Wengine wanawaza ni kuchukua mzigo mahali, kuongeza cha juu kidogo na kisha kutafuta mteja na kumuuzia kile kitu na kisha kupata faida, na mzunguko kuendelea hivyo hivyo kila wakati. Ni sawa kabisa, ila kwangu mimi Roho mtakatifu aliniambia kuwa biashara ni; ***"Nguvu, na Uwezo wa rohoni wa kushawishi na kuwavuta watu kuja kwako kununua bidhaa au kupata huduma tena bila kuwalazimisha."***

Biashara kiroho ni zaidi ya kuuza na kununua, ni zaidi ya kwenda Kariakoo, China au Uturuki, na kuchukua bidhaa na kuja Tanzania kuzipandisha bei na watu kununua kwa bei kubwa kuliko uliyonunulia.

Biashara ni kutoa huduma au bidhaa na kisha kulipwa malipo stahiki. Lakini pia biashara haiishii tu katika kuuza na kununua bidhaa bali mtu anaweza kutoa huduma kwa kipaji au taaluma aliyonayo au kipawa alichojaliwa na Mungu na kisha kupata malipo stahiki.

Biashara sio kuwa na vyeti vya darasani vinavyoonesha kuwa wewe umesomea biashara au ni mbobezi wa biashara. Ukichunguza sana watu wengi walio na mafanikio makubwa katika biashara sio kwamba ni wasomi sana au wana elimu kubwa. Ila ni watu ambao walijua siri na kanuni chache za kufanikiwa kibiashara na kuamua kuziishi na ndio hizo zilizowapa matokeo makubwa hata sasa.

Kiufupi zaidi, biashara ni kitu chochote halali ambacho mtu hufanya kwa lengo la kujipatia kipato au kujiongezea kipato maana wapo watu ambao wameajiriwa lakini bado wanajishughulisha na biashara.

Japokuwa tumeokoka lakini hatuishi katika dunia yetu tofauti bali tunaishi na watu wengine lakini pia pamoja na kuwa tumeokoka

maisha yetu yanapaswa kuendelea kama kawaida. Ada za watoto zinatakiwa kulipwa, bili za maji na umeme, huduma za usafiri na mengine mengi ya kijamii, kuvaa, kula, kulipa karo ni vitu vinavyotakiwa kuendelea kama kawaida. Kwa sababu hii wengi wetu hujikuta tunaingia katika sekta ya biashara.

## 1.2 MKRISTO NA BIASHARA

Wakati mwingine inawawia vigumu sana watumishi wa Mungu na hasa wachungaji kuwa huru kuwafundisha watu makanisani juu ya biashara kwa maana kwa baadhi ya madhehebu imekuwa ngumu sana kuelewa kuwa hata wakristo wanaweza kufanya biashara kama watu wengine. Lakini pia watu wengi wana imani mbaya juu ya elimu ya fedha na biashara kwa wakristo na kuamini kuwa yeyote anayetoa mafundisho ya namna hiyo sio wa Mungu. Na baadhi ya waalimu wa Neno hawaamini katika mafanikio na hasa mafanikio ya kifedha na hii ni hofu tu ambayo hutokana na uhaba wa maarifa na mafunuo ya Neno la Mungu.

Labda nikukumbushe kitu kimoja kuwa; kwenye Biblia wapo watu na watumishi wa Mungu wakubwa ambao walikuwa na fedha na mali nyingi sana na wala haikuharibu mahusiano yao na Mungu.

Tunasoma habari za Ayubu katika kitabu cha;

**Ayubu 1:1-4**

**“Palikuwa na mtu katika nchi ya Usi, jina lake alikuwa akiitwa Ayubu; mtu huyo alikuwa mkamilifu na mwelekevu, ni mmoja aliyemcha Mungu, na kuepukana na uovu. Kisha walizaliwa kwake wana saba, na binti watatu. Mali yake nayo yalikuwa ni kondoo elfu saba, na ngamia elfu tatu, na jozi za ng’ombe mia tano, na punda wake mia tano, na watu wa nyumbani wengi**

**sana; basi hivi mtu huyo alikuwa ni mkuu sana kuliko watu wote wa upande wa mashariki. Nao wanawe huenda na kufanya karamu katika nyumba ya kila mmoja wao kwa siku yake; nao wakatuma na kuwaita maumbu yao watatu ili waje kula na kunywa pamoja nao."**

> ***"Watu wanaomjua Mungu hapa duniani ndio watu wanaotakiwa kuwa na nguvu kiuchumi na mafanikio makubwa kifedha kuliko watu wengine wote."***

Ukisoma vizuri utagundua kuwa Biblia inamuongelea Ayubu kama mtu aliyekuwa mtakatifu na ambaye hakuwahi hata kwa siku moja kumtenda Mungu dhambi. Lakini pamoja na utakatifu wake bado aliweza kumiliki na kuwa na mali nyingi. Sasa hii elimu ambayo watu wameaminishwa kuwa kuokoka ni kuwa duni imetoka wapi?

Imani kama hizi ndio imefanya leo hii kanisa la Mungu na watu wake wamekuwa na maisha ya duni na umaskini wa hali ya juu. Yaani inawezekanaje watu wa milki ya shetani wawe na nguvu kiuchumi kuliko sisi tunaosema tunamjua Mungu?

Hivyo sio dhambi kwa mkristo yeyote kufanya biashara na ni kawaida sana kwa mlokole au mkristo kuwa mfanyabiashara na kuwa tajiri.

Hata Yesu mwenyewe katika mafundisho aliyokuwa anatoa kwa wanafunzi wake aliongea kwa mafumbo juu ya kufanya biashara na kuwekeza.

Tunasoma katika kitabu cha;

**Luka 19:12-26**

**"Basi akasema, Mtu mmoja, kabaila, alisafiri kwenda nchi ya mbali, ili ajipatie ufalme na kurudi. Akaita watu kumi katika watumwa wake, akawapa mafungu kumi ya fedha, akawaambia, Fanyeni biashara hata nitakapokuja. Lakini watu wa mji wake walimchukia, wakatuma wajumbe kumfuata na kusema, hatumtaki huyu atutawale. Ikawa aliporudi, ameupata ufalme wake, aliamuru waitwe wale watumwa aliowapa fedha, ili ajue faida aliyopata kila mtu kwa biashara yake.**

**Akaja wa kwanza, akasema, Bwana, fungu lako limeleta faida ya mafungu kumi zaidi. Akamwambia, Vema, mtumwa mwema; kwa vile ulivyokuwa mwaminifu katika neno lililo dogo, uwe na mamlaka juu ya miji kumi. Akaja wa pili, akasema, Bwana, fungu lako limeleta mafungu matano faida. Akamwambia huyu naye, Wewe uwe juu ya miji mitano. Akaja mwingine akasema, Bwana, hili ndilo fungu lako, ambalo nililiweka akiba katika leso. Kwa maana nilikuogopa kwa kuwa u mtu mgumu; waondoa usichoweka, wavuna usichopanda.**

**Akamwambia, nitakuhukumu kwa kinywa chako, mtumwa mwovu wewe. Ulinijua kuwa ni mtu mgumu, niondoaye nisichoweka, na kuvuna nisichopanda; basi, mbona hukuiweka fedha yangu kwa watoao riba, ili nijapo niipate pamoja na faida yake? Akawaambia waliosimama karibu, Mnyang'anyeni hilo fungu, mkampe yule mwenye mafungu kumi. Wakamwambia, Bwana, anayo mafungu kumi. Nawaambia, kila aliye na kitu atapewa, bali yule asiye na kitu atanyang'anywa hata alicho nacho."**

Kwahiyo hata watu waliookoka wanaweza kufanya biashara na kupata mafanikio makubwa sana katika biashara zao hizo.

## 1.3 TOFAUTI KATI YA MFANYABIASHARA MKRISTO NA WA KAWAIDA

Nini kinachomtofautisha mfanyabiashara mkristo na yule asiyeokoka?

Baadhi ya tofauti hizo ni pamoja na hizi zifuatazo;

- Misingi ya biashara zao.

Tofauti ya kwanza inayotofautisha kati ya mfanyabiashara mkristo na yule wa kawaida ni misingi waliyoitumia katika kuanzisha biashara zao. Kiuhalisia kila mtu anayeanza biashara huwa anaanza na msingi wake.

Sasa kwa wale watu wa duniani wengi misingi yao huwa ni kweye nguvu za giza na kutoa kafara kwa miungu yao ili waweze kufanikiwa katika biashara zao. Kwa sisi tuliookoka na kumjua Mungu msingi wa biashara zetu huwa ni Mungu mwenyewe.

Msingi mzuri ndio utakaoamua biashara yako idumu au isimame. Kwahiyo tofauti ya kwanza inayowatofautisha watu hawa wawili katika ulimwengu wa biashara ni misingi yao.

Neno la Mungu linasema katika kitabu cha;

**Mathayo 7:24-27**

**"Basi kila asikiaye hayo maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba. Na kila asikiaye hayo maneno yangu asiyafanye, atafananishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga; mvua ikanyesha, mafuriko**